***Soma vifungu vifuatavyo. Vina nafasi 1 hadi 15. Kwa kila nafasi umepewa majibu manne. Chagua jibu lifaalo kati ya yale uliyopewa.***

Wahenga ____1____ waliposema kuwa____2____. Watahiniwa wengi huandika insha ____3____ mithili ya vipofu pasi na kutambua ____4____ uandishi wa insha. Kama yalivyo maswali mengine katika mitihani ____5____ uandishi wa insha vilevile ni ____6____ kujibiwa kwa kuzingatia ____7____ yanayotolewa kabla ya swali lenyewe. Jambo la ajabu ni kwamba, wengi wa wanafunzi huanza tu kuandika ____8____ ya kuisoma sehemu hii muhimu. Amri ya mtahini ni muhimu sana na ni sharti ifuatwe kikamilifu.

1. A. hawakukosea B. walikosea C. hawakutuandaa D. walituandaa

2. A. asiyekujua hakuthamini B. kuyumbayumba sio kuanguka C. mla nawe hafi nawe ila mzaliwa nawe D. jambo usilolijua ni usiku wa kiza

3. A. kitamaduni B. kilevi C. kipopo D. kijuzi

4. A. sintofahamu inayoikumba B. suitafahamu inayoukumba C. suitafahamu inayoikumba D. sintofahamu inayoukumba

5. A. ; B. , C. : D. ?

6. A. maswali ambalo yanafaa B. swali ambalo halifai C. maswali ambayo hayafai D. swali ambalo linafaa

7. A. mashauri B. maonyo C. maagizo D. ushauri

8. A. minghairi ya B. sembuse C. maadamu D. mintarafu

Fisi alikuwa amezoea ____9____ kwa muda mrefu sana. Maisha yake ya kuiparamia ____10____ na wanyama wengine yalikuwa yamemshinda. Hii ni ____11____ wanyama kama simba na chui waliyateketeza mabaki ya mawindo yao. Aliamua kuanza kufanya ____12____. Alitengeneza silaha kama mishale ili kuwawinda wanyama wengine; jambo ambalo lilikuwa limepingwa vikali na mfalme wao. Tendo hilo lilikuwa ____13____. Juhudi zake ____14____ kwani mishale yake ilikuwa ____15____ na haingemudu kumfuma mnyama yeyote.

9. A. kuvuna mahali ambapo hakupanda B. kupanda mahali ambapo alivuna C. kupanda kabla ya kwenda kuvuna D. kuvuna mahali ambapo alipanda

10. A. vyakula vilivyoliwa B. mizoga iliyosazwa C. wanyama waliouwawa D. nyama zilizoliwa

11. A. kwasababu B. kwakuwa C. kwa sababu D. kwa minajili

12. A. jambazi B. ujambazi C. ujangili D. jangili

13. A. halali B. lilikataliwa C. likiharamia D. haramu

14. A. hazikufua dafu B. zilizaa matunda C. hazikuambulia patupu D. zilifua dafu

15. A. si butu B. butu C. kali D. bora

23. Andika sentensi ifuatayo bila kirejeshi **-amba-**

***Mfanyakazi ambaye atafanya bidii atapandishwa madaraka.***

A. Mfanyakazi afanyaye bidii atapandishwa madaraka.

B. Atakayefanya kazi kwa bidii atapandishwa madaraka.

C. Mfanyakazi ambaye atakayefanya kazi kwa bidii atapandishwa madaraka.

D. Mfanyakazi anayefanya kazi kwa bidi atapandishwa madaraka.

24. Ni upi wingi wa sentensi hii?

***Ubavu wa mnyama wangu umevunjwa na jirani mwenye wivu.***

A. Ubavu wa wanyama wangu umevunjwa na majirani wenye wivu.

B. Mbavu za wanyama wetu zimevunjwa na majirani wenye wivu.

C. Ubavu za wanyama zangu zimevunjwa na jirani wenye wivu.

D. Mabavu ya wanyama wetu yamevunjwa na jirani wenye wivu.

25. Kama juzi ilikuwa Jumatano tarehe kumi na nane, mtondo itakuwa siku gani tarehe ngapi?

A. Jumatatu tarehe ishirini na tatu

B. Alhamisi tarehe ishirini na tisa

C. Jumapili tarehe ishirini na mbili

D. Ijumaa tarehe ishirini.

26. Ni sentensi ipi yenye maana sawa na

***Si nadra wao hutembeleana.***

A. Wao hutembeleana mara chache

B. Wao hutembeleana mara nyingi

C. Si mara kwa mara wao hutembeleana

D. Kutembeleana kwao ni adimu

27. Ni methali gani yenye maana sawa na:

**Ngoja ngoja huumiza mtu matumbo?**

A. Asiyesikia la mkuu huvunjika guu

B. Pole pole ndio mwendo

C. Chelewa chelewa utakuta mwana si wako

D. Haraka haraka haina baraka

28. Chagua sentensi iliyotumia sitiari.

A. Maua ni sungura siku hizi.

B. Moyo wake ulimshauri asikate tamaa.

C. Alice alijifungua salama salimini.

D. Ondigo ni mweusi mithili ya masizi.

29. Andika sentensi ifuatayo katika kauli ya kutendewa.

***Kaguai alienda uwanjani akaucheza mpira.***

A. Mpira ulichezwa na Kaguai uwanjani.

B. Kaguai aliuchezea mpira uwanjani.

C. Mpira ulichezwa na Kaguai.

D. Uwanjani ulichezwa mpira na Kaguai.

30. Makao ya mchwa si

A. kingulima

B. kinyago

C. kishirazi

D. kichuguu

